JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

MAGAZETINI WIKI HII

Mji wa Serikali, Mtumba S.L.P. 315, DODOMA. Simu: +255 26 2310021 Barua pepe: km@sheria.go.tz



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana (kulia), akizungumza na ujumbe wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), jijini Dodoma jana. Kushoto ni Rais wa TLS, Wakili Harold Sungusia. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Andengenye aagiza vyeti vya kuzaliwa wapewe wanaostahili

**Na FADHILI ABDALLAH,** *Kigoma*

MKUU wa Mkoa Kigoma, Thobias Andengenye, amesema usajili na utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano unaofanyika mkoani hapa, hauna uhusiano na utoaji wa hadhi ya uraia wa Tanzania kwa wageni na wakimbizi.

Andengenye alisema hayo katika semina ya mafunzo kwa viongozi waandamizi wa serikali wakiwemo wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa, viongozi wa dini na wazee kwa lengo la kuwajengea uwezo kutumia nafasi zao kuhamasisha jamii kushiriki jambo hilo.

Alisema inafahamika Kigoma ina wakimbizi na idadi kubwa ya wageni na wahamiaji kutoka nchi za ukanda wa maziwa makuu, lakini operesheni ya utoaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano inayosimamiwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), haina uhusiano na utoani hadhi ya uraia kwa wageni.

Aliagiza kuzingatiwa kwa upembuzi na upekuzi wa nyaraka muhimu uzingatiwe kuhakikisha wanaopewa vyeti vya kuzaliwa ni wenye sifa tu.

Katika hotuba hiyo iliyotolewa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Michael Ngayarina, Andengenye alisema mpango huo utaleta manufaa makubwa mkoani Kigoma kwa kuwa na idadi ya watoto ambao watatoa taswira nzuri katika kupanga mipango ya maendeleo.

Awali, Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali kutoka RITA, Irene Lesulie, alisema mpango huo unalenga kusajili na kutoa vyeti kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano waliozaliwa nchini na hilo linatokana na kuwepo kwa idadi ndogo ya watoto waliosajiliwa na kupata vyeti ikilinganishwa na waliozaliwa.

Akitoa takwimu za idadi ya watoto waliozaliwa na kupata vyeti, Lesulie alisema mwaka jana watoto 442,662 walizaliwa Kigoma na kati yao 46,480 walisajiliwa na kupata vyeti sawa na asilimia 10 ya watoto hao.

Mpango wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano ulianza mwaka 2013 na hadi hivi sasa watoto milioni 8.6 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa katika mikoa 24.

Kwa upande wake, Mwakiklishi wa Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mariam Mkumbwa aliwataka watendaji wanaosimamia operesheni hiyo kuhakikisha taarifa zinazokusanywa zinaingizwa katika mifumo watoto wanaosajiliwa na kupewa vyeti wasomeke mahali popote nchini.

# Bunge laagiza sheria ndogo zenye dosari zirekebishwe

**Na Ikunda Erick, Dodoma**



BUNGE limeagiza mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya katiba ya nchi zifanye marekebisho ya sheria hizo.

Pia, mamlaka hizo zimeagizwa ziwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya bunge kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo Oktoba 02, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Jasson Rweikiza (pichani) alilieleza bunge wakati akiwasilisha taarifa kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika mkutano wa 10 na 11 na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika mkutano wa nane na tisa.

Rweikiza alisema uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge ulionesha kuwa maazimio kuhusu dosari 19 kati ya 85 ambazo ni sawa na asilimia 22.89 ya dosari zote hayajatekelezwa.

Alisema mchanganuo wa maazimio hayo unaonesha kuwa, maazimio kuhusu dosari 16 yanagusa sheria ndogo zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na maazimio matatu ni kuhusu sheria ndogo inayosimamiwa na Wizara ya Madini.

Rweikiza alisema maazimio hayo ambayo hayajatekelezwa yanahusu dosari katika sheria ndogo 10 ambazo ni Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022, Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Mji wa Bunda ya Mwaka 2022.

Nyingine Sheria Ndogo ya (Ada na Vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022, Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Stendi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022, Sheria Ndogo ya (Ada ya Ukusanyaji na Uzoaji Taka) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022.

Pia imo Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ya Mwaka 2022, Sheria Ndogo ya (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ya Mwaka 2022 na Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ya Mwaka 2022.

Sheria nyingine ni Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya

Wilaya ya Misungwi ya Mwaka 2023; na Kanuni ya Madini ya mwaka 2022.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk Pindi Chana alisema serikali inafanya marekebisho na maboresho ya sheria ili tume ya marekebisho ya sheria iwe inazipitia sheria kabla ya kuwasilishwa bungeni.

Waziri wa Tamisemi, Mohamed Mchengerwa alisema wizara hiyo itahakikisha mifumo na kanuni na sheria zenye ukinzani zinafanyiwa maboresho kwa wakati.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk Eliezer Feleshi alisema serikali inaendelea kufanya maboresho ya mifumo ikiwemo kitengo cha uandishi wa sheria.

Mbunge wa Nkasi, Aida Khenan (Chadema) alisema sheria ndogo zinapaswa zikaguliwe kabla ya kutumika kwa sababu zinasababisha madhara kwa wananchi.

Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina (CCM) alisema ni muhimu kuwe na sheria moja ya kuongoza halmashauri zote ili kuwepo na usawa na kuondoa changamoto na dosari zinazojitokeza.

# TCD yataka 'viraka' Katiba ya 1977 vizibwe kabla ya uchaguzi 2024/25

**Na Halfani Chusi**

KITUO cha Demokrasia Tanzania (TCD), kimeishauri serikali kufanya mabadiliko madogo katika Katiba ya sasa ili kuwa na Tume huru ya Uchaguzi itakayowezesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kufanyika kwa uhuru, haki na ushiriki mpana wa demokrasia.

Kituo hicho kimetoa ushauri huo baada ya kubaini serikali imechelewa kuanzisha mchakato wa upatikanaji Katiba Mpya na kuna uwezekano isipatikane kabla ya uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa kituo hicho, Prof. Ibrahimu Lipumba, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salama, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maazimio ya mkutano wa wadau wa kitaifa kujadili hali ya demokrasia nchini kuelekea uchaguzi wa 2024-25 uliofanyika kwa siku mbili mfululizo Agosti 22 na 23 mwaka huu.

Kiongozi huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), aliyataja maazimio hayo kuwa ni pamoja na Serikali kukubali misaada ya kuimarisha utendaji wa tume kutoka kwa washirika wa maendeleo kama vile UNDP na wengine.

"Vyama vya siasa Zanzibar, viendeleze utashi wa kisiasa katika utekelezaji wa kudumisha dhana ya maridhiano kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, uchaguzi wa Zanzibar ufanyike kwa siku moja ili wadau wa demokrasia waweze kuandaa mkutano wa hali ya demokrasia kwa upande wa Zanzibar ili kudumisha dhana ya maridhiano na utatuzi wa changamoto kwa pamoja.

"Pia, serikali iwezeshe na kusaidia majadiliano baina ya vyama vya siasa, asasi za kiraia na mashirika ya kiserikali ili kuhakikisha kunakuwa na mtazamo wa pamoja katika kujenga dhana ya ushirikiano kushinda kwa hoja bila kupingwa," alisema.

Prof. Lipumba aliyataja maazimio mengine ni kuwekeza uhuru wa kutoa maoni na kujieleza kwa wananchi, viongozi vyama vya siasa na asasi za kiraia, vyama vya siasa viwe na kanuni zinazoelezea na kuongoza mchakato wa uteuzi wa wagombea wa nafasi za viti maalum vya wanawake zinazoakisi misingi ya uwazi, usawa na demokrasia.

"Fedha zilizotengwa na serikali kwa ajili ya elimu kuhusu Katiba ya mwaka 1977, zipelekwe kwa asasi za kiraia na elimu hii iwe endelevu katika mchakato mzima wa mabadiliko ya katiba, taarifa ya Jaji (Joseph) Warioba na viambatanisho vyake hususani randama, zitumiwe katika elimu kuhusu katiba.

"Pia ninashauri, muswada wa mabadiliko ya katiba upelekwe pamoja na muswada wa Tume huru ya Uchaguzi katika mkutano ujao wa Bunge kama ilivyofanyika mwaka 1992 wakati wa kuridhia mfumo wa vyama vingi.

"Muda uliobakia kuelekea uchaguzi ni mfupi. Mkutano wa kitaifa wa maridhiano uliofanyika Aprili 2022 Dodoma, ulijadili na kuwasilisha serikalini muswada wa mfumo wa sheria ya uchaguzi huru na wa haki," alisema.

Mkutano huo uliokutanisha vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu nchini, ulifanyika Agosti 22 na 23 mwaka huu.

# Wanaotoa msaada wa kisheria wapewa somo

MAKAMU wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Profesa Muhammed Awadelkarim Elhussein amewataka wadau wanaotoa msaada wa kisheria Zanzibar, kuzingatia sheria wakati wanapotekeleza kazi zao kuepusha ukiukwaji wa haki za binadamu.

Profesa Elhussein alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wasaidizi wa sheria na wadau wa haki za binadamu katika ukumbi wa chuo kikuu cha Zanzibar.

Alisema haki za binaadamu zinatambulika katika dini, lakini zinaendelea kukiukwa, hivyo kila mmoja anapaswa kutimiza wajibu wake katika kuwatetea watu na kuheshimu sheria za nchi.

Profesa Elhussein alisema msaada wa kisheria ni sehemu ya haki za binadamu na kutokana na hilo, chuo hicho kimeamua kuwajengea uwezo wasaidizi wa sheria watambue utaratibu na sheria zinazowasimamia katika utoaji wa huduma hiyo kwa jamii.

Alieleza eneo hilo la utoaji wa msaada wa kisheria bado lipo chini kutokana na kukosa rasilimali watu, hivyo ameishauri serikali kuwawekea utaratibu maalumu watu wanaotoa msaada wa kisheria iwe ni sehemu ya ajira katika shehia zao.

Kwa upande wake mkuu wa kitengo cha sheria kutoka ZU, Dk. Sikujua Omar Hamdani alisema licha ya kutolewa elimu ya sheria katika maeneo mbalimbali, bado ipo haja ya kutolewa elimu zaidi hususan katika maeneo ya vijijini kuiwezesha jamii inayoishi katika maeneo hayo kuzijua sheria na haki zao.

Aliongeza kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na idara ya katiba na msaada wa kisheria Zanzibar, kipindi cha mwaka 2021/22 jumla ya wananchi 163,260 wamepewa elimu ya sheria katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba.

# Govt commits to improve law making process

From RODGERS LUHWAGO

THE government plans to review the Law Reform Commission of Tanzania Act so that the commission can fully participate in the process of enacting laws in the country, the Parliament has been informed.

Contributing to the report from the Parliamentary Standing Committee on Subsidiary Legislations tabled yesterday on the analysis of various bylaws enforced by various authorities in the country and the implementation of parliamentary resolutions reached in previous Bunge meetings, Minister for Legal and Constitutional Affairs, Dr Pindi Chana said the ministry plans to improve the process of enacting laws and the bylaws to reduce anomalies.

She said there is a pressing need for the Law Reform Commission to carry out thorough research on the pros and cons of any legislation before being brought to the Parliament for scrutiny.

During the 10th and 11th parliamentary meetings the House scrutinised various bylaws after which it directed respective government authorities to rectify some shortcomings noted.

According to Committee Chairman, Jason Rweikiza, the Parliament reached resolutions, with some directives being issued to some ministries after scrutinising a number of bylaws submitted to the House during the 8th and 9th Parliamentary meetings.

According to Mr Rweikiza, despite the resolutions reached, the respective government institutions and authorities did not rectify the anomalies in the bylaws and regulations that Members of Parliament said had detrimental effects to the public.

The committee chair said Bunge resolutions on 19 shortcomings out 83, which is equivalent to 22.89 per cent of all anomalies, were yet to be implemented, an indication that some government institutions and authorities are undermining the powers vested upon the Legislature.

Mr Rweikiza said the resolutions on 16 shortcomings touched on bylaws supervised and enforced by the Office of President (Regional Administration and Local Government) while three resolutions on three anomalies had to do with bylaws enforced by the Ministry of Minerals.

The committee chair mentioned the bylaws whose anomalies had not been rectified as including the bylaw on environmental health and sanitation of 2022 enforced by Ikungi District Council, the environmental health and sanitation of 2022 enforced by Bunda Township Council and recreational permits and fee of 2022 enforced by Msalala District Council,

Other bylaws include those that deal with collection of bus stand levy imposed by Msalala District Council, garbage collection also imposed by Msalala District Council, administration of fee and levy issues enforced by Mvomero District Council and environmental health and sanitation enforced by Temeke Municipal Council, Nsimbo District Council,Misungwi District Council and the Mining (State Participation) Regulations, 2022 (TS No. 574.

# Rita kuzindua mpango wa uhamasishaji usajili watoto

Na Fadhili Abdallah, Kigoma

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) unatarajia kuzindua mpango wa uhamasishaji wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano ili waweze kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Hayo yameelezwa katika semina ya siku moja kwa viongozi waandamizi wa serikali ili kuweza kutumia nafasi zao kuhamasisha jamii kushiriki kwenye utaratibu huo.

Naibu Kabidhi Mkuu wa serikali Rita, Irene Lesulie alisema mpango huo unalenga kusajili na kutoa vyeti kwa watoto wote chini ya miaka mitano waliozaliwa nchini na hiyo inatokana na idadi ndogo ya watoto waliosajiliwa na kupata vyeti ukilinganisha na watoto waliozaliwa.

Lesulie alisema kwa mwaka jana watoto 442,662 walizaliwa mkoani Kigoma ambapo kati yao ni watoto 46,480 waliosajiliwa na kupata vyeti ikiwa ni asilimia 10 ya watoto waliozaliwa.

Mpango wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano ulianza mwaka 2013 ambapo mpaka sasa jumla ya watoto milioni 8.6 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa katika mikoa 24 nchini.

Akizungumza wakati akifungua semina hiyo, Mkuu wa Mkoa Kigoma, Thobias Andengenye alisema kuwa mpango huo utaleta manufaa makubwa kwa mkoa kuwa na idadi ya watoto ambao watatoa taswira nzuri katika kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo mkoani humo.

Katika hotuba iliyotolewa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya Buhigwe, Michael Ngayarina alisema kuwa pamoja na umuhimu huo ametaka watendaji wa serikali wanaosimamia utaratibu huo kuhakikisha taratibu za upekuzi na utambuzi za watu wanaopaswa kupewa vyeti hivyo zinazingatiwa.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mkurugenzi Msaidizi huduma za ustawi wa jamii Tamisemi, Mariam Mkumbwa ametaka watendaji wanaosimamia utaratibu huo kuhakikisha taarifa zinazokusanywa kuingizwa kwenye mifumo ili watoto wanaosajiliwa na kupewa vyeti waweze kusomeka kwenye mifumo mahali popote nchini.

# Bunge lapitisha muswada marekebisho ya sheria

**Na SELINA MATHEW,** ***Dodoma***

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2023 ambao unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbili.

Sheria hizo ni Kanda Maalumu za Uwekezaji kwa Mauzo Nje ya Nchi, Sura ya 373 na Sheria ya Kanda Maalumu za Kiuchumi, Sura ya 420.

Akiwasilisha muswada bungeni, jana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, alisema kuwa, umegawanyika katika sehemu tatu ambapo ya kwanza, inahusu mashartiua utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika muswada.

Jaji Feleshi alisema sehemu ya pili na tatu, zinapendekeza marekebisho ya sheria ya Kanda Maalumu za Uwekezaji kwa mauzo nje ya nchi, Sura ya 373 na sheria ya Kanda Maalumu za Sheria 420.

Alifafanua kuwa, sheria hizo zinarekebishwa katika vifungu vya 2 na 3, mtawalia kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya neno 'Waziri'.

Alieleza kuwa pamoja na marekebisho ya tafsiri ya neno waziri, kifungu cha 14, kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta neno 'responsible for industries'.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alisema kuwa lengo la marekebisho ni kuhakikisha sheria husika, zinatekelezwa na waziri mwenye dhamana na masuala husika kwa mujibu wa hati idhini ya mgawanyiko wa majukumu ya mawaziri ambayo hutolewa na Rais.

Alisema kwa sasa, sheria hizo zinamtafsiri waziri kama waziri mwenye dhamana ya viwanda, ilihali jukumu la usimamizi wa masuala hayo, yanahamishiwa Ofisi ya Rais-Mipango na Uwekezaji.

Kwa mujibu wa Jaji Feleshi, hatua hiyo itaondoa ulazima wa kufanya marekebisho katika sheria kila yanapotokea mabadiliko katika wizara.

Akisoma maoni na ushauri wa kamati, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Florent Kyombo, alieza kuwa, wameuchambua na kuujadili muswada huo kwa kuzingatia, katiba, sheria mbalimbali na kanuni za kudumu za Bunge.

Alibainisha kuwa, katika kutekeleza jukumu hilo, kamati hiyo ilikutana na serikali jana na kupokea maelezo ya mwanasheria mkuu wa serikali kuhusu maudhui ya muswada huo.

"Kamati imeridhika kwamba, marekebisho yanayopendekezwa, yatasaidia utekelezaji bora wa sheria zinazohusika, yamezingatia hati idhini ya mgawanyo wa majukumu ya mawaziri ambayo hutolewa na Rais," alisema.

Alisema kamati imekubaliana na mapendekezo ya muswada yaliyowasilishwa na mwanasheria mkuu wa serikali kwa kuwa, yanalenga kuhakikisha sheria zinazorekebishwa, zinaendana na muundo na majukumu kulingana na hati idhini ya mgawanyo wa majukumu ya mawaziri iliyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Juni 22, 2023 katika Gazeti la Serikali Na. 407B.

Alieleza kuwa majukumu hayo ya usimamizi wa masuala ya uwekezaji ambayo awali yalikuwa kwa waziri wa viwanda, biashara na uwekezaji, sasa yanahamishiwa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji.

"Kamati inaipongeza serikali kwa hatua hiyo ya kuleta marekebisho hayo muhimu kwa lengo la kuboresha ufanisi na uendeshaji wa majukumu ya ofisi hiyo," alisema.